## RIPOTI YA KAMATI YA MAWASILIANO, ARDHI NA NISHATI YA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

## SEHEMU YA KWANZA

### 1. UTANGULIZI

Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati ya Baraza la Wawakilishi ni miongoni mwa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi Zanzibar iliyoanzishwa kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar kifungu cha 85 ya mwaka 1984 na Kanuni ya 107 (1) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, (Toleo la 2020).

Majukumu ya Kamati hii ya kudumu yameorodheshwa kwenye Jadweli la Kwanza la Kanuni za Baraza la Wawakilishi kama ifuatavyo:

i. Kufatilia utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyotolewa katika Ripoti ya Kamati ya mwaka uliotangulia;

ii. Kufatilia utekelezaji wa sera na mipango ya Wizara husika kwa kadri Spika atakavyoelekeza kwa mujibu wa malengo yaliyowasilishwa Barazani wakati wa usomaji kwa Bajeti na hotuba nyengine za Wizara alizotoa katika Baraza;
iii. Kufatilia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Kitaifa na miradi ya wananchi ya Wizara husika;
iv. Kuchunguza na kufatilia mapato na matumizi ya kila mwaka ya Serikali na kama matumizi yaliyofanywa yalizingatia thamani halisi ya fedha;
v. Kuchambua mapendekezo ya Serikali kuhusu makadirio ya Wizara husika ya mapato na matumizi ya kila mwaka;
vi. Kushughulikia miswada ya sheria itakayokabidhiwa kwake na Spika;
vii. Kuchambua ahadi zote za Wizara zilizo chini ya Kamati kama zitakavyokuwa zikitolewa katika Baraza ns kufuatilia utekelezaji wa ahadi hizo;
viii. Kufikiria jambo jengine lolote litakalopelekwa kwake na Spika.

Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati mbali ya majukumu yake yaliyoainishwa kwa mujibu wa Kanuni lakini pia ina jukumu la kufatilia utekelezaji wa wizara tatu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ikiwemo Mashirika, Mamlaka na Vitengo vilivyomo ndani ya Wizara hizo. Wizara zinazosimamiwa na Kamati hii ni:-

(1) Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi
(2) Wizara Ardhi na Maendeleo ya Makaazi
(3) Wizara ya Maji, Nishati na Madi

## 1.1 MUUNDO WA KAMTI

Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati imeundwa na Wajumbe saba (7) na makatibu wawili (2), orodha ya Wajumbe na Makatibu ni kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe Yahya Rashid Abdullah | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe Hudhaima Mbaraka Tahir | Makamo Mwenyekiti |
| 3. | Mhe Mussa Foum Mussa | Mjumbe |
| 4. | Mhe Fatma Mohammed Ramadhan | Mjumbe |
| 5. | Mhe Kombo Mwinyi Shehe | Mjumbe |
| 6. | Mhe Rukia Omar Ramadhan | Mjumbe |
| 7. | Mhe Bahati Khamis Kombo | Mjumbe |
| 8. | Ndg. Rahma Kombo Mgeni | Katibu |
| 9. | Ndg. Himid Haji Choko | Katibu |

## 1.2 MALENGO NA MUDA WA KAZI ZA KAMTI

Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati ilifanya kazi zake kwa kufata malengo yafuatayo:

(a) Kufatilia maagizo yaliyotolewa katika ripoti ya Kamati ya mwaka 2019/2020.

(b) Kufatilia ahadi za Serikali zilizotolewa katika Mkutano wa Bajeti wa Mwaka 2021/2022.

(c) Kufatilia utekelezaji wa Bajeti (kwa kazi za Kawaida na kazi za Maendeleo) kwa mwaka 2021/2022.

(d) Kufatilia ukusanyaji wa mapato katika vitengo vya Serikali pamoja na kufanya ziara kwa Taasisi zake.

Vile vile katika mwaka wa fedha 2021/2022 Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati ilifanya kazi zake kwa muda wa wiki kumi (10) kwa mizunguko mitano (5) kama ifuatavyo: -

(i) Unguja kuanzia tarehe 18/01/2021 hadi tarehe 29/01/2021
(ii) Pemba na Unguja kuanzia tarehe 29/03/2021 hadi tarehe03/04/2021
(iii) Unguja kuanzia tarehe 09/8/2021 hadi tarehe 20/08/2021
(iv) Pemba na Unguja kuanzia tarehe 8/11/2021 hadi tarehe 19/11/2021
(v) Tanzania Bara na Unguja kuanzia tarehe 17/1/2022 hadi tarehe 28/1/2022

### 1.3 NJIA NA MBINU ZILIZOTUMIKA

Katika kuhakikisha kamati inatekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kwa mujibu wa Kanuni, Kamati ilitumia njia na mbinu mbali mbali ikiwemo; -

*(i)* Kufanya vikao na Wizara pamoja na Taasisi zilizo chini ya Wizara husika kwa lengo la kupata taarifa juu mambo au maswala mahsusi ambayo Kamati ilipenda kupata taarifa zake kutoka kwa watendaji wa taasisi hizo.

*(ii)* Kufanya ziara za ukaguzi katika miradi ya Maendeleo, sehemu za kazi na sehemu nyengine ambazo kwa namna moja ama nyengine zinahusika na utekelezaji wa majukumu ya Wizara husika.

*(iii)* Kufanya mikutano na Wafanyakazi pamoja na Wadau kwa lengo la kupokea maoni juu ya masuala mbali mbali ambayo Kamati ilikuwa inayafanyia kazi.

### 1.4 HADIDU REJEA

Katika Utekelezaji wa kazi kwa mwaka 2021/2022 Kamati ilitumia hadidu rejea zifuatazo; -

a) Katiba ya Zanzibar ya Mwaka 1984.
b) Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977
c) Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la Mwaka 2020.
d) Hansard za Baraza za Mwaka 2021/2022,
e) Hotuba za Bajeti za Wizara zinazosimamiwa na Kamati hii.

## SEHEMU YA PILI

## WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA UCHUKUZI

## 2.0 MUUNDO WA WIZARA.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa sasa inaundwa na Idara tatu (3), Afisi kuu Pemba (Taasisi hii inaratibu majukumu ya Wizara kwa upande wa Pemba) pamoja na Tasisi nane (8) zinazojitegemea.

Idara za Wizara ni Idara ya Utumishi na Uendeshaji, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti na Idara ya Mawasiliano. Taasisi zinazojitegemea ni: -

(i) Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani,
(ii) Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar,
(iii) Mamlaka ya Usafiri Baharini,
(iv) Shirika la Bandari Zanzibar,
(v) Shirika la Meli Zanzibar,
(vi) Wakala wa Barabara Zanzibar,
(vii) Wakala wa Serikali wa Karakana Kuu ya Magari Zanzibar
(viii) Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA Zanzibar.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi inatekeleza majukumu yake kupitia program kuu tatu (3) na program ndogo nane (8) kama ifuatavyo: -

## 2.1 PROGRAMU KUU YA KWANZA: MIUNDOMBINU NA HUDUMA ZA USAFIRISHAJI.

Programu hii ina jukumu la kuhakikisha miundombinu na huduma za usafiri zilizobora, salama na endelevu zinapatikana katika sekta ya usafirishaji hapa Zanzibar. Programu hii inatekekelezwa kupitia Programu ndogo tatu kama ifuatavyo: -

### (a) PROGRAMU NDOGO YA KWANZA: USIMAMIZI WA USAFIRISHAJI.

Programu ndogo hii inasimamiwa na Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani, Wakala wa Serikali wa Karakana Kuu ya Magari Zanzibar Pamoja na Mamlaka ya Usafiri Baharini ambayo ina lengo la kuhakikisha

usafiri wa nchi kavu na baharini unakuwa bora na salama muda wote kwa Unguja na Pemba.

**(i) MAMLAKA YA USAFIRI NA USALAMA BARABARANI.**

Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani kupitia programu ndogo ya Usimamizi wa Usafirishaji, ina jukumu la kudhibiti usalama wa watumiaji wa barabara pamoja na utoaji wa huduma za usafiri wa barabara.

**CHANGAMOTO ZA MAMLAKA YA USAFIRI NA USALAMA BARABARANI**

(1) Ufinyu wa bajeti inayopatiwa Mamlaka katika utekelezaji wa majukumu yake jambo ambalo hupelekea baadhi ya masuala ya msingi kutofanyika.

(2) Ukosefu wa gari kwa matumizi ya ofisini, Mamlaka inakabiliwa na ukosefu wa gari kwa Unguja na Pemba ampapo imekua changamoto katika utekelezaji wa kazi zao za usimamizi wa kazi barabarani.

(3) Uwepo wa deni kubwa inalodaiwa Mamlaka kutokana na kukopa kwa nyaraka zinazotumika kutolea huduma za usafiri barabarani na kupelekea kusimamishwa kupewa huduma ya kupatiwa nyaraka hizo za kufanyia kazi kutoka Wakala wa Uchapaji Zanzibar.

(4) Ufinyu na ubovu wa ofisi za Mamlaka kwa Upande wa Pemba.

(5) Uwepo wa madeni yanayotokana na maslahi ya wafanyakazi (overtime& perdiem)

(6) Kuwepo kwa mfumo unaoruhusu benki moja kwa ajili ya malipo (PBZ) na malipo hayo kulazimika kutanguliwa na utolewaji wa control number inayopatikana katika eneo moja tu na kusababisha foleni kubwa na msongamano.

(7) Maagizo ya Serikali ya kuwepo vituo maalum kwa ajili ya ukaguzi wa gari zinazopakia na zinazoendeshwa na wageni kwa lengo la kuwapunguzia usumbufu, ambapo imepelekea kutoa mwanya kwa wanaojihusisha na biashara hiyo kutofuata utaratibu na kupelekea gari hizo na wageni kutumia nyaraka za kughushi.

(8) Kamati imegundua kuwepo kwa tabia kwa madereva wa Serikali kutokua na leseni kitu ambacho ni kinyume na sheria za usalama barabarani.

(10) Uhaba wa wakaguzi wa magari kwa upande wa Pemba.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI KWA MAMLAKA YA USAFIRI NA USALAMA BARABARANI.**

(1) Kamati inaishauri Wizara kuangalia suala zima la kuongezewa bajeti Mamlaka ili iweze kutekeleza kazi zake kwa ufanisi na kuweza kukamilisha malengo waliojipangia.

(2) Pia kamati inashauri kupatiwa usafiri Mamlaka ili iweze kutekeleza kazi zake kwani kazi zao kwa asilimia kubwa zinahitaji usafiri.

(3) Kutokana na deni kubwa wanalodaiwa Mamlaka kamati inashauri Wizara kufanya jitihada za makusudi kulipa deni hilo ili waweze kupatiwa nyaraka zinazohitajika katika kutekeleza kazi zao kutoka Wakala wa Uchapaji.

(4) Kamati imesikitishwa na uwepo wa changamoto ya mfumo uliopo wa kutumia benki moja inayokwaza jitihada za Mamlaka, hivyo Kamati inaitaka Wizara kulichukulia hatua suala hili na kulitatua kwa kufikiria hatua mbadala zitakazopunguza changamoto iliopo sasa ambayo inaathiri katika utendaji kazi.

(5) Kamati vile vile inashauri kuangaliwa na kuchukuliwa hatua suala la madeni ya wafanyakazi wa Mamlaka ambalo limekua linarudisha nyuma jitihada za wafanyakazi hao ambao wanategemewa katika kufanikisha utendaji kazi wa mamlaka.

(6) Hata hivyo, kamati inaitaka Wizara kuangalia uwezekano wa kupatiwa ofisi au kufanyiwa matengenezo iliyopo ili kuwa katika hali nzuri kwa upande wa Pemba.

(7) Kamati inashauri kuwe na utaratibu wa kutolewa leseni za *manual* na *automatic* ili kwenda sambamba na hali halisi ambayo hivi sasa

vyombo vingi viliopo ni automatic na kuacha utaratibu wa kuwatathmini madereva kwa kutumia manual pekee ambapo vyombo hivyo kwa sasa vimeanza kupungua kimatumizi.

**(ii) MAMLAKA YA USAFIRI BAHARINI**

Mamlaka ya Usafiri Baharini ina jukumu la kusimamia usafiri wa baharini ikiwemo kusimamia usalama na ulinzi wa vyombo vya baharini, kusimamia shughuli za ukaguzi na usajili wa meli, utoaji wa leseni kwa vyombo vidogo vidogo, utoaji wa leseni za manahodha na wahandisi wa vyombo vidogo vidogo, utoaji wa hati na vitambulisho vya mabaharia, kusimamia shughuli za upakiaji wa abiria katika bandari za Zanzibar, kudhibiti uchafuzi wa mazingira ya baharini na utekelezaji wa kanuni ya kimataifa ya ulinzi wa meli na bandari (ISPS Code).

**CHANGAMOTO INAYOIKABILI MAMLAKA YA USAFIRI BAHARINI (ZMA)**

(1) Ukosefu wa kikosi kazi cha uokozi (search and rescue organization) ambacho ni muhimu sana kuwepo bandarini na ni changamoto kubwa kukosekana kwake.
(2) Kukosekana kwa vifaa vya utafutaji na uokozi kama vile boti na vifaa vya mawasiliano, hii inatokana na gharama kubwa ya kununua vifaa hivyo hali ambayo inaleta changamoto wakati ambapo litatokea tatizo.
(3) Kukosekana kwa wafanyakazi wataalamu kutokana na maslahi madogo yaliyopo katika Mamlaka kitu ambacho kinawavunja moyo wataalamu waliopo.
(4) Kukabiliwa na matayarisho hafifu ya utekelezaji wa IMO AUDIT (III CODE) ‘CORRECTIVE ACTION PLAN’ CAP, hali hii inatokana na ukosefu mkubwa wa fedha kuweza kukamilisha mataarisho hayo.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI KWA MAMLAKA YA USAFIRI BAHARINI (ZMA)**

(1) Kamati inaishauri Wizara kuangalia uwezekano na kuomba kurudishiwa ruzuku kutoka Serikalini ili iweze kujiendesha na kutatua baadhi ya changamoto ambazo kwa sasa wanashindwa kutokana na uhaba wa fedha.

(2) Pia, kamati inashauri Mamlaka kuendelea na ufatiliaji na usajili wa vyombo vidogo vidogo kwa ajili ya usalama na kuweza kukusanya mapato yatakayosaidia Mamlaka hii.

(3) Kamati inashaiuri Mamlaka kuchukua jitihada za makusudi kuhakikisha wana wafanyakazi wenye ujuzi lakini pia kuwaangalia maslahi yao ili yaweze kwenda sambamba na taalamu zao.

(4) Vile vile kamati inaishauri Mamlaka kupitia Wizara kufanya jitihada za kupatikana vifaa vya utafutaji na uokozi kutokana na umuhimu wake kutoka Serikalini ama kwa wafadhili ili kuepusha athari itokanayo na kukosekana kwa uwepo wa vifaa hivyo.

(5) Kamati inashauri kuchukuliwa hatua suala la uwepo wa kikosi kazi cha uokozi (search and rescue organization) kutokana na umuhimu wake.

**(iii) WAKALA WA SERIKALI WA KARAKANA KUU YA MAGARI ZANZIBAR.**

Wakala wa Serikali wa Karakana Kuu ya Magari kupitia Programu ndogo ya Usimamizi wa Usafirishaji imepewa jukumu la kuzifanyia matengenezo Gari za Serikali na Binafsi kupitia Karakana zake zilizopo Unguja na Pemba.

**CHANGAMOTO ZA WAKALA WA SERIKALI WA KARAKANA KUU YA MAGARI ZANZIBAR.**

(1) Kukosekana kwa wataalamu mahiri wa gari za kisasa, ambapo kamati imejuilishwa kwa sasa Wakala imeazima fundi kutoka JKU kutokana na kusitishwa uajiri Serikalini.
(2) Wakala kutoweza kutumia mapato yake hali inayopelekea kushindwa kujiendesha.
(3) Ukosefu na Upungufu wa vifaa vya kufanyia kazi.

(4) Kamati imegundua mazingira ya kazi hayakua rafiki kiafya na kiutendaji.
(5) Uhaba wa wateja kwa Karakana.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI KWA WAKALA WA SERIKALI WA KARAKANA KUU YA MAGARI ZANZIBAR.**

(1) Kamati inashauri kuchukuliwa jitihada za makusudi kwa bajeti ijayo kuweza kupatikana wataalamu wa magari ili waweze kusaidia na kufanikisha kazi za Karakana Kuu ya Serikali ili kufikiwa lengo la kuundwa kwake.
(2) Katika suala la mapato wanayokusanya Karakana kamati inaishauri Wizara kufatilia na kuweza kupatiwa asilimia ambayo wataweza kuitumia katika kuendeshea kazi zao za kila siku ikiwemo ununuzi wa vifaa vya magari vinavyohitajika.
(3) Kamati inaishauri Wizara kuiangalia Karakana Kuu ya Serikali katika bajeti ijayo kwa kuwatengea fedha za ununuzi wa vifaa ili iweze kujiendesha na kufanikisha kazi zake kama ilivyokusudiwa.
(4) Kamati inashauri Wizara kuibadilisha karakana Unguja na Pemba na kuwa katika mazingira rafiki na yatakayowezesha kuleta ufanisi katika kazi kwa kuiboresha.
(5) Vile vile kamati inaishauri wizara kuchukua jitihada za makusudi kuiwezesha Karakana kuinuka ili iweze kutumika kwa kutoa huduma na kuingiza kipato.

**(b) PROGRAMU NDOGO MIUNDOMBINU YA USAFIRISHAJI**

Programu hii inasimamiwa na Wakala wa Barabara Zanzibar pamoja na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Programu hii ina lengo la kuhakikisha kuwepo kwa miundombinu ya usafirishaji iliyosalama na endelevu.

**(i)WAKALA WA BARABARA ZANZIBAR.**

Wakala wa barabara imepewa jukumu la kujenga, kutunza na kuzifanyia matengenezo barabara mbalimbali Unguja na Pemba ili ziweze kupitika

muda wote. Kamati katika kazi zake imetembelea barabara mbali mmbali Unguja na Pemba na Mtambo wa Lami uliopo Vitongoji Pemba na Kibele Unguja.

**CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI WAKALA WA BARABARA ZANZIBAR.**

(1) Ufinyu wa bejiti katika kutekeleza miradi ya ujenzi wa barabara.

(2) Uelewa mdogo wa wananchi katika kulinda hifadhi ya barabara

(3) Uvamizi wa hifadhi ya barabara

(4) Ukosefu wa vifaa vya kazi kwa wajenzi wa barabara ikiwemo nguo na vifaa vya kujikinga.

(5) Mpango wa muda mrefu wa ujenzi wa daraja la Uzi Ng'ambwa ambao unaathiri wakaazi wa eneo hilo.

(6) Changamoto ya ulipaji fidia kwa wananchi inayotokana na ujenzi wa barabara ambayo inasababisha Serikali kuwa na deni kubwa litokanalo na ujenzi wa barabara kwa Unguja na Pemba.

(7) Ukosefu wa baadhi ya spare, ukosefu wa walinzi katika eneo, na ukosefu wa uzio kwa Mtambo wa Lami wa Vitongoji ambapo kamati imejuilishwa kuwa ni agiza la Mhe Rais kuwekwa uzio eneo hilo na hadi sasa halijatekelezwa**.**

(8) Ukosefu wa hatimiliki kwa eneo la mtambo wa Kibele na Vitongoji ambapo umepelekea kuanza kuvamiwa na wananchi.

(9) Kamati imegundua kuwepo na changamoto katika suala zima la mipango miji na vijiji Unguja na Pemba ambapo inaleta athari wakati wa ujenzi wa barabara.

(10) Barabara nyingi hasa za mjini kuwa na mashimo hali amabayo inaleta usumbufu kwa watumiaji na kuleta taaswira mbaya kwa nchi.

(11) Ukosefu wa alama za barabarani kwa baadhi ya barabara Unguja na Pemba

(12) Ukosefu wa service kwa vifaa vya mitambo

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI KWA WAKALA WA BARABARA**

(1) Kamati inashauri Wizara kuangalia umuhimu wa kuwapatia bajeti inayokidhi wakala wa barabara ili waweze kufanikisha malengo waliojipangia.

(2) Kamati inaishauri Wizara kupitia Wakala wa Barabara kutumia wataalamu wenye ujuzi pamoja na kuwa na mipango ya muda mrefu wakati wa ujenzi wa barabara ili tuwe na barabara zenye ubora na zinazokidhi haja kimatumizi kwa muda mrefu na kuacha kufanya kazi kwa mazoea.

(3) Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi, Wizara ya Maji, Nishati na Madini na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kuangaliwa na kuchukuliwa hatua zinazofaa katika suala zima la mipango miji na vijiji kwa kuwekwa utaratibu mara tu baada ya kupimwa viwanja kuwekwa miundombinu ya maji, umeme na barabara ili kuepuka changamoto zinazotokea sasa wakati wa ujenzi wa barabara na kusabisha madeni makubwa ya fidia kwa Serikali.

(4) Kamati inashauri wakati wa ujenzi barabara kuwekwa roada reseved area ambazo zitasaidia kuzuia wananchi kujenga katika maeneo hayo ya barabara.

(5) Kamati inashauri kufanyiwa kazi suala la uwekaji wa alama za barabarani zenye kudumu muda mrefu katika barabara zote Unguja na Pemba.

(6) Vile vile kamati inapendekeza kufanywa jitihada za kufanyiwa usafi barabara zote kwa kushirikiana na Halmashauri ili kuzitunza kwa kukatwa majani, kupandwa bustani ma kusafishwa mitaro ili kuwa katika hali nzuri.

(7) Kamati inasisitiza kuangaliwa suala la kupatiwa vifaa vya kufanyia kazi wajenzi wa barabara ikiwemo nguo na vifaa maalum vya

kujikinga wakati wakiwa kazini ili kuwa salama kiafya na kuepuka athari ikiwemo kuungua na lami imoto.

(8) Vile vile kamati inashauri Serikali kuwa makini zaidi kwa ujenzi wa barabara za ndani zinazotaka kujengwa ili kuepuka uharifu wa miundombinu iliyopo ikiwemo maji na umeme wakati wa ujenzi huo.

(9) Pia, kamati inasikitishwa na kuchelewa kwa ujenzi wa daraja la Uzi Ng'ambwa ambapo ni kilio cha muda mrefu kwa wakaazi wa eneo hilo na ni ahadi ya muda mrefu kwa Serikali hivyo, Kamati inaishauri Serikali izidi kutoa kipaumbele kwa ujenzi wa mradi huu.

(10) Kamati pia inashauri kufanywa jitihada ili kupatikana hatimili kwa eneo la mitambo Unguja na Pemba ili kuepusha kuvamiwa.

(10) Pia, kamati inashauri kupatiwa mafunzo watendaji waliopo katika mitambo ili kuweza kuiendesha kwa ufanisi na kuweza kutatua changamoto zitakazojitokeza wakati wa ufanyaji kazi kwa kuepusha athari za uharibifu kwa mitambo ambayo ni ya gharama kubwa.

(11) Kamati pia inashauri kuendelea kutumiwa kwa mitambo ya zamani ambayo bado inaweza kufanya kazi ili iendelee kusaidia kuzalisha lami kwa wingi na kusaidia kuleta ufanisi katika utekelezaji wa kazi.

(12) Vile vile kamati inaitaka Wizara kupitia Wakala wa Barabara kuwa na utaratibu wa kuvifanyia service vifaa vya mitambo ili kuepeuka kuharibika mapema.

**(c) PROGRAMU NDOGO YA TATU: HUDUMA ZA USAFIRISHAJI**

Programu hii inasimamiwa na Shirika la Bandari, Shirika la Meli na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege ambazo zimepewa jukumu la kuhakikisha kuwepo kwa huduma bora za usafirishaji wa abiria na mizigo katika sekta ya usafiri wa Bahari na Anga.

**(i) SHIRIKA LA BANDARI - ZANZIBAR.**

Shirika la Bandari lina jukumu la kutoa huduma za bandari ikiwemo huduma za meli na majahazi na huduma za mizigo. Kamati katika kazi zake

imaefanikiwa kutembelea bandari ya Wete, bandari ya Mkoani, Bandari ya Malindi, Bandari ya Mkokotoni, mnara wa kuongozea meli Kigomasha, Mnara wa Mangapwani na Mnara wa Nungwi.

**CHANGAMOTO INAYOLIKABILI SHIRIKA LA BANDARI ZANZIBAR**

**Bandari ya Wete**

(1) Kuwepo kwa kina kidogo cha maji jambo ambalo linapelekea vyombo kushindwa kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.
(2) Kuwepo kwa gati ndogo isiyokidhi mahitaji.
(3) Matumizi makubwa ya bandari hii kwa watu wa visiwa Jirani
(4) Upungufu wa wafanyakazi wataalamu
(5) Ukosefu wa ofisi za wafanyakazi wa bandari.

**Bandari ya Mkoani**

1. Kutoweza kupokea meli zinazobeba makontena kutokana na miundombinu kutokua sawa kwa sasa.

**Bandari ya Malindi**

1. Ufinyu wa bandari ambao unapelekea kuwepo na changamoto ya maeneo ya kukaa makontena.

**Bandari ya Mkokotoni**

1. Ufinyu wa ofisi za kudumu kwa vitengo viliopo bandarini hapo.
2. Ukosefu wa hatimiliki ambapo imejuilishwa kamati kuwa hadi sasa Shirika wanalipia leese tu ambayo ni gharama kutokana na kutopatiwa hatimiliki walioomba kutoka Wizara ya Ardhi.
3. Ukosefu wa usafiri wa uhakika kwa wafanyakazi waliopo ambao wengi wao wanaishi mjini.
4. Ukosefu wa vifaa vya hospitali kama vile vitanda, dawa na gari ya wagonjwa.

**Mnara wa Kigomasha, Mangapwani na Nungwi**

1. Kukosekana kwa huduma ya maji ya uhakika na umeme kwa mnara wa Kigomasha ambapo kwa sasa shirika linapeleka huduma ya maji kwa kutumia gari na kwa umeme mnara unatumia umeme wa nguvu za jua (solar power)
2. Ukosefu wa uzio kwa eneo la minara hali inayolekea kuvamiwa na wananchi.
3. Ukosefu wa hatimiliki wa eneo la mnara wa Mangapwani na Nungwi
4. Uvamizi wa maeneo ya minara

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI**

(1) Kamati inashauri watendaji wa bandari wazidi kuunga mkono juhudi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kufikia uchumi wa kati kupitia sekta ya usafirishaji na mizigo.

(2) Aidha, Kamati inalitaka Shirika likae na litafakari kwa kina changamoto ya kushuka kwa mapato ya bandari Pemba na kuchukua hatua zinazofaa katika kuhakikisha mapato yanaongezeka.

(3) Pia, kamati inashauri kuwepo mpango kazi ambao utaenda sambamba na matumizi ya bajeti ya muda mrefu kwa upande wa Pemba.

(4) Vile vile, bandari kwa kushirikiana na ZMA wakubaliane juu ya utoaji ruhusa wa vyombo vidogo vidogo vinavyochukua abiria ili kulinda usalama wa raia na mali zao.

(5) Kamati inalishauri shirika kuchagua miradi yenye tija kwa muda mrefu na yenye kutekelezeka.

(6) Shirika litafute Hatimiliki za maeneo yake ili uepusha kuvamiwa na wananchi.

(7) Katika ujenzi wa miradi, Kamati inashauri Bandari ya Wete ipewe kipaumbele katika ujenzi wake kwani ni tegemeo kwa uingizaji mapato.

(8) Vile vile, Kamati inaishauri Wizara kuhakikisha linafikiwa lengo la mradi wa ujenzi wa bandari ya Mkoani ambayo pia itaiwezesha

Serikali kuongeza mapato kupitia bandari hiyo mara baada ya kuanza kazi.

(9) Kamati inapongeza ujenzi wa bandari ya Mkokotoni uliokamilika kwa asilimia 95 lakini pia inashauri kukamilishwa kwa maeneo mengine yaliyobakia ikiwemo sehemu ya kupitia abiria, kuwekwa uzio, barabara na sehemu za kuhifadhia mizigo ili iweze kufanya kazi kama ilivyokusudiwa na kuiingizia fedha Serikali zitokanazo na makusanyo na tozo.

(10) Kamati inashauri utengenezwe utaratibu mzuri wa kukusanya mapato kwa Bandari ya Mkokotoni kuweza kuzuia uvujaji wa mapato na kupelekea hasara kwa Serikali.

(11) Kamati pia inashauri kuwepo na wafanyakazi wa kutosha kwa vitengo vyote muhimu kwa bandari ya Mkokotoni ambao wataiwezesha bandari kufanya kazi kama ilivyokusudiwa ikiwepo ZRB, UHAMIAJI, POLISI, na AFYA.

(12) Suala la uhaba wa ofisi za vitengo, kamati inashauri kuangaliwa na kuchukuliwa hatua za dharura ili kuhakikisha wanapatiwa ofisi za kudumu na usafiri wa uhakika.

(13) Kamati inashauri kupatiwa vifaa hospitali iliyopo katika eneo la bandari ya Mkokotoni ili kuweza kusaidia kuwatumikia watumiaji wa eneo hilo pindi wanapohitaji huduma za afya.

(14) Vile vile kamati inaitaka Wizara kupitia Shirika la Bandari kufatilia suala la upatikanaji wa hatimiliki ya eneo la Bandari ya Mkokotoni ili kuepusha changamoto ya uvamizi kwa wananchi waliopo maeneo hayo.

(15) Kamati inashauri kuimarishwa ulinzi na usalama kwa bandari ya Wete kutokana na matumizi makubwa yaliopo kwa bandari hiyo.

(16) Kamati inatoa wito kwa Wizara kupitia Shirika la Bandari kuziimarisha Bandari zake zote ikiwemo kuharakisha ujenzi wa bandari ya mpya Mangapwani ambayo itasaidia kwa kiasi kikubwa kutatua changamoto za kibandari ziliopo hivi sasa.

**(ii) SHIRIKA LA MELI ZANZIBAR**

Shirika la Meli Zanzibar limepewa jukumu la kuendesha meli zote za Serikali pamoja na kutoa huduma za uwakala kwa meli za Kigeni zinazoingia katika bandari za Zanzibar. Kamati katika kutekeleza majukumu yake imeweza kutembelea meli ya Mv Mapinduzi II na MT Ukombozi II

**CHANGAMOTO ZA SHIRIKA LA MELI ZANZIBAR**

(1) Bajeti isiyokidhi katika kuendesha kazi za Shirika
(2) Uhaba wa maafisa wa meli wenye umahiri katika uendeshaji wa meli za shirika
(3) Uhaba wa wataalamu wa shirika wenye umahiri kwa shughuli za uendeshaji meli
(4) Uwezo mdogo wa shirika wa kulipa madeni kutokana na gharama kubwa za utengenezaji na uendeshaji wa meli, hivyo Shirika kushindwa kutekeleza majukumu yake kikamilifu.
(5) Kutokuwepo na mfumo maalum wa mishahara ya ubaharia na kutotambulika katika taasisi za kiutumishi za Serikali.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI KWA SHIRIKA LA MELI**

(1) Kamati inaishauri Serikali kuliangalia Shirika kwa kulipatia bajeti itakayokidhi katika utendaji wa kazi zao ili Shirika liweze kujiendesha, kwani kwa muda mrefu limeshindwa kujiendesha kutokana na ukosefu wa fedha na changamoto za Meli zinazomilikiwa na Shirika kuwa na hitilafu za mara kwa mara.
(2) Kamati inashauri kuangaliwa kwa jicho la pekee suala zima la kupatiwa mafunzo maafisa wa meli ili waweze kufanya kazi kwa ufanisi na kuendana na mabadiliko ya utumiaji wa vyombo vya kisasa.
(3) Kamati inashauri Shirika kuwa na mpango maalum wa kusomesha mabaharia wake ambao wana uwezo wa kusoma. Aidha, kamati inalitaka Shirika katika bajeti ijayo kuwa na fungu maalum ambalo

litatumika kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa watendaji na mabahria kwa fani za muda mfupi na muda mrefu ili kuondokana na changamoto ya ukosefu wa mafunzo.

(4) Pia, kamati inalitaka shirika kufatilia na kuchukua hatua zinazofaa kuhakikisha wanaweka sawa mfumo mzuri kwa mishahara na maslahi ya mabaharia ambao utatambulika katika taasisi za kiutumishi Serikalini.

(5) Kamati inahimiza kutekelezwa maagizo yaliyotolewa na Serikali kuhusiana na kuuzwa kwa meli zake zisizofanya kazi ili kupunguza hasara inayopatikana kwa kuendelea kuwepo kwake.

**(iii) MAMLAKA YA VIWANJA VYA NDEGE – ZANZIBAR**

Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar ina jukumu la kuviendesha, kuvisimamia, na kuvitunza viwanja vya ndege vya Serikali Unguja na Pemba kwa kuzingatia miongozo na kanuni za kitaifa na kimataifa. Kamati ilipata fursa ya kutembelea Uwanja wa ndege AAKIA, Uwanja wa ndege Kigunda na Uwanja wa ndege Pemba.

**CHANGAMOTO ZA MAMLAKA YA VIWANJA VYA NDEGE – ZANZIBAR**

(1) Ufinyu wa nafasi na uchakavu wa majengo ya Mamlaka Terminal II

(2) Uchakavu na uhaba wa magari kwa Unguja na Pemba

(3) Uvamizi wa baadhi ya maeneo ya viwanja vya ndege kwa Unguja na Pemba

(4) Ukosefu wa mafundi wa mashine za ukaguzi

(5) Uchache wa wafanyakazi kwa viwanja vya Unguja na Pemba

(6) Uhaba wa maeneo ya kukaa abiria wakati wa kushuka abiria Termina II

(7) Ukosefu wa hatimiliki kwa viwanja vyote Unguja na Pemba, ambapo wameijuilisha kamati kuwa kwa sasa viwanja hivyo vinalipa leese kitu ambacho hakiko sawa kwao.

(8) Uhaba wa wafanyakazi wataalamu

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI**

1. Mamlaka iandae mpango maalum utakao wasaidia watendaji kupata bima ya afya – NHIF
2. Aidha, Kamati inashauri tahadhari ziongezwe zaidi katika kuwalinda wafanyakazi wa sekta ya aviation katika usalama wao
3. Vile vile, mamlaka ifanye juhudi za makusudi za kuwalinda watumishi wake na maradhi mbali mbali yakiwemo magonjwa ya kupumua.
4. Vile vile Kamati inasisitiza kukamilishwa suala la upatikanaji wa hatimili kwa viwanja vyote Unguja na Pemba.
5. Kamati pia, inasisitiza kuchukuliwa hatua suala la kupatikana wafanyakazi wataalamu ambao wataiwezesha Mamlaka kufanyakazi kwa ufanisi na kutoa huduma stahiki na zenye viwango.
6. Kamati pia inasisitiza kupatikana kwa mafundi wa mashine za ukaguzi ambao watasaidia kuzitunza, kurekebisha na kuzifanyia uchunguzi wa mara kwa mara mashine hizo.
7. Kamati inashauri kwa jengo la abiria terminal II kuangaliwa njia mbadala ili liweze kutumika ipasavyo na kuondoa chanagamoto ziliopo sasa ikiwemo uhaba wa eneo la abiria hali ambayo inaleta shida kwa watumiaji.
8. Vile vile kamati inaitaka Mamlaka kupitia Wizara ya Uchukuzi, Miundombinu na Mawasiliano kuhakikisha wanaweka uzio kwa viwanja vya ndege Unguja na Pemba ili kuzuia kuvamiwa na wananchi.
9. Pia, kamati inashauri kuchukuliwa hatua za makusudi kutenganisha mizigo ya safari za ndani na nje ya nchi ili kuondokana na usumbufu uliopo sasa ikiwemo mrundikano wa abiria wanaousubiri mizigo na hali halisi ya magonjwa ya uviko 19.

**2.2 PROGRAMU KUU YA PILI: MIUNDOMBINU NA HUDUMA ZA TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO (TEHAMA)**

Programu hii ina lengo la kuhakikisha huduma bora na endelevu za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) zinapatikana kwa muda wote hapa nchini. Programu hii inatekekelezwa kupitia Programu ndogo mbili kama ifuatavyo: -

**(a) PROGRAMU NDOGO YA KWANZA: USIMAMIZI WA MIUNDOMBINU YA TEHAMA.**

Programu hii inasimamiwa na Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA Zanzibar. Taasisi hii imepewa jukumu la kusimamia na kuendesha Mkonga wa Taifa wa Mawasiliano wa Zanzibar, Kituo kikuu cha kuhifadhia taarifa pamoja na Minara ya mawasiliano ya simu. Lengo kuu la programu hii ni kuhakikisha kuwepo kwa miundombinu bora ya Mawasiliano iliyosalama na endelevu.

**CHANGAMOTO ZA WAKALA WA MIUNDOMBINU YA TEHAMA**

1. Kuwepo na uharibifu wa miundombinu ya Mkonga wa Taifa ambayo unarejeshesha nyuma jitihada za Serikali na kuitia hasara.
2. Uhaba wa bajeti

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI**

1. Kamati inashauri kutolewa zaidi elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa Mkonga wa Taifa na kuchukuliwa hatua kwa atakaebainika amefanya hujuma kwa kukata ama kuiba nyaya.

**(b) PROGRAMU NDOGO YA PILI: USIMAMIZI WA HUDUMA ZA TEHAMA.**

Programu hii inasimamiwa na Idara ya Mawasiliano na ina lengo la kuhakikisha matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano yanaongezeka kwa taasisi zote pamoja na kutoa matumizi sahihi ya utumiaji wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kwa wananchi Idara imeendelea kuratibu huduma za mawasiliano ya simu, internet na Posta Zanzibar.

## 2.3 PROGRAMU KUU YA TATU: UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA UCHUKUZI.

Progamu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Ujenzi Mawasiliano na Uchukuzi ina lengo la kuhakikisha kuwa Wizara inatayarisha mipango bora na usimamizi mzuri wa rasilimali watu. Programu hii inatekekelezwa kupitia Programu ndogo tatu kama ifuatavyo: -

### (a) PROGRAMU NDOGO YA KWANZA: UTAWALA NA UENDESHAJI

Programu hii inasimamiwa na Idara ya Utumishi na Uendeshaji ambayo ina lengo la kuimarisha huduma za ofisi na usimamizi wa rasilimali watu katika sekta ya Mawasiliano na Uchukuzi.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI**

1. Kamati inaishauri Wizara kuandaa mahitaji ya wafanyakazi wanaohitajika katika Idara na Taasisi ziliopo chini yake wa fani mbali mbali na kupeleka Serikalini kwa ajili ya kupatiwa ili waweze kuziba pengo liliopo la ukosefu wa wataalamu ambalo linakwaza na kurudisha nyuma juhudi za wizara. **katika utekelezaji wa majukumu ya ofisi na kupunguza ufanisi.**
2. Vile vile kamati inaishauri Wizara kuwa na mpango maalum kwa kila mwaka wa fedha kwa ajili ya kusomesha watendaji wa ofisi kwa masomo ya muda mfupi na muda mrefu ili waongeze ujuzi ambao watautumia katika kuleta mafanikio kwa Wizara.

### (b) PROGRAMU NDOGO YA PILI: URATIBU WA MIPANGO, SERA NA TAFITI ZA WIZARA

Programu hii ndogo inasimamiwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti na ina lengo la kuhakikisha mipango na sera za Wizara zinatekelezwa. Huduma zinazotolewa katika programu hii ndogo ni uandaji na uibuaji wa sera na tafiti, utayarishaji na utekelezaji wa bajeti ya Wizara pamoja na uandaaji na usimamizi wa mpango mkakati wa Wizara.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI**

1. Kamati inaishauri Wizara kupitia Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kupitia wataalamu wake kuhakikisha wanaandaa na kuwa na mipango ya muda mrefu katika miradi inayotekelezwa na wizara ikiwemo barabara ili kuepusha hasara ya kurudiwa kwa miradi hiyo baada ya kipindi kifupi na kuisababishia Serikali hasara ya fedha nyingi ambazo zingeweza kutumika katika kuleta maendeleo kwenye sekta nyengine.
2. Vile vile kamati inashauri Idara kuandaa bajeti yenye kukidhi na kuleta tija kwa Serikali ambayo itaweza kufanikisha malengo waliojiwekea kwa kila mwaka wa fedha.
3. Kamati pia, inashauri Wizara kuhakikisha wanaandaa mipango yenye kutekelezeka kwa mujibu wa hali itakavyoruhusu na kuachana na tabia ya kuandaa mambo mengi ambayo yanashindwa kutekelezeka.

### (c) PROGRAMU NDOGO YA TATU: URATIBU WA SHUGHULI ZA WIZARA PEMBA

Programu hii inasimamiwa na Ofisi Kuu – Pemba ambayo ina lengo la kuhakikisha majukumu ya Wizara yanatekelezwa kwa upande wa Pemba. Huduma inayotolewa katika programu hii ni uratibu wa kazi za Wizara Pemba ikiwemo kusimamia shughuli za utawala na utumishi, mipango na bajeti, huduma za usafiri na TEHAMA pamoja na ujenzi na matengenezo ya barabara mbali mbali – Pemba.

### CHANGAMOTO ZA URATIBU WA SHUGHULI ZA WIZARA PEMBA

1. Uchakavu wa jengo la ofisi ya Pemba na kupelekea baadhi ya ofisi kuhamwa kutokana na ubovu.
2. Mrundikano wa madeni ya fidia za nyumba pamoja na vipando kwa barabra zilizojengwa muda mrefu.
3. Upungufu wa upatikanaji fedha za kuendeshea kazi hali inayopelekea kutotekelezwa shughuli za ofisi kama ilivojipangia.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI**

1. Kamati inaishauri Wizara kuchukua hatua za kukarabati jengo la Ofisi Pemba kwa bajeti ijayo ili waweze kulitumia na kuondokana na changamoto iliyopo ya kuhama ambayo inaathiri utendaji kazi wa Ofisi.
2. Pia kamati inaishauri wizara kuchukua hatua madhubuti na kutoa kipaumbele kwa Ofisi ya Pemba kwa kuhakikisha upatikanaji wa fedha unakua mzuri na kwa wakati ili Ofisi iweze kutekeleza majukumu iliojipangia.
3. Kamati inasikitishwa na madeni makubwa yaliopo ya fidia za nyumba na vipando kwa Unguja na Pemba yanayotokana na ujenzi wa barabara, hivyo, kamati inaishauri Wizara kuangalia mbinu mbadala kuweza kulipa na kuondokana na madeni makubwa yaliopo kwa wananchi.

Kamati kupitia ziara zake ilipata fursa ya kutembelea TTCL na POSTA Dar es Salaam na kujifunza mambo mbali mbali

**SHIRIKA LA POSTA TANZANIA**

Shirika la Posta linatoa huduma mbali mbali ikiwemo;

- Kutoa huduma za Posta ndani na nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
- Kutosheleza mahitaji ya kitaifa ya huduma za Posta za Viwanda, Biashara na jamii kwa ujumla ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
- Kutoa huduma za kutuma na kulipa fedha kwa njia ya hawala za Posta (Money Order, Postal Order) au kwa kutumia njia nyingine zinazoonekana zinafaa ndani na nje ya nchi; nk

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI**

1. Kamati inatoa wito kwa Shirika la Posta kuendelea kutolewa elimu na kujenga uelewa kwa Wananchi wa Zanzibar ili waweze kuitumia Posta kwa manufaa ya kijamii na Kiuchumi hasa juu ya matumizi ya Posta na huduma wanazotoa.
2. Kamati imeridhishwa na mashirikiano yaliopo baina ya Posta Tanzania Bara na Posta Visiwani na inashauri kuzidi kuendelezwa mashirikiano hayo ili huduma hii iwe yenye kuleta tija kwa nchi na faida kwa watumiaji.
3. Kamati pia, imefurahishwa na mipango ya Shirika ya kuwa na Kituo cha Huduma Pamoja kwa Zanzibar ambacho kitasaidia kurahisisha huduma mbali mbali za kijamii ikiwemo upatikanaji wa vyeti vya kuzaliwa itapatikana kimtandao kupitia huduma hii.
4. Pia, kamati imefarajika na uwepo wa Duka Mtandao ambalo linasaidia sana wajasiriamali kuuza bidhaa zao kwa urahisi kupitia duka mtandao, hivyo, kamati inashauri

**SHIRIKA LA SIMU TANZANIA TTCL**

Shirika la Simu Tanzania lina majukumu ikiwemo kusimamia na kuendesha huduma zote za mawasiliano ndani na nje ya nchi, kuimarisha usalama wa taifa kupitia mawasiliano na kutoa huduma ya miamala ya kifedha kupitia simu za mkononi.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI**

1. Kamati inashauri kutolewa elimu kwa wananchi juu ya huduma zitolewazo na TTCL ili waweze kuwa na uelewa na waweze kutumia huduma zao za mawasiliano.
2. Pia kamati inaendelea kusisitiza kuendeleza mashirikiano kati ya Taasisi na Serikali zetu Tanzania Bara na Zanzibar ili kukuza huduma zitolewazo kwa pande zote.

## WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI

### 3.0 UTANGULIZI

Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi ni miongoni mwa Wizara 16 zilizoundwa kupitia "Legal Notice No.14" ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ya tarehe 12 Disemba, 2020 ambayo imeainisha Wizara, Majukumu ya Wizara na Taasisi zitakazounda Wizara husika. Aidha, Wizara hii ina dhamana ya kuhakikisha kwamba wananchi wote wa Zanzibar wanapata makaazi bora, salama na nafuu.

### 3.1 MUUNDO WA WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI

Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi inajumuisha Idara na Taasisi zifuatazo: -

i. Idara ya Mipango Sera na Utafiti,
ii. Idara ya Uendeshaji na Utumishi,
iii. Ofisi Kuu Pemba,
iv. Kamisheni ya Ardhi (COLA),
v. Mahakama ya Ardhi,
vi. Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali,
vii. Wakala wa Majengo Zanzibar (ZBA) na
viii. Shirika la Nyumba Zanzibar (ZHC)

Aidha, Wizara inazo Bodi Tendaji (Executive Boards) tano (5) ambazo ni:-

i. Bodi ya Uhaulishaji Ardhi,
ii. Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba,
iii. Bodi ya Kondominio,
iv. Bodi ya Usajili wa Wakandarasi na
v. Bodi ya Usajili wa Wahandisi, Wasanifu na Wakadiriaji Majengo.

Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi inatekeleza majukumu yake kupitia Programu Kuu 2 ambazo ni;

i. Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi.
ii. Programu ya Usimamizi wa Ardhi na Makaazi

### 3.2 PROGRAMU KUU: UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA ARDHI

Programu hii ina jukumu la kuratibu utekelezaji wa kazi za Wizara na inajumuisha Programu ndogo tatu ambazo zinatekelezwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, Idara ya Utumishi na Uendeshaji na Afisi Kuu Pemba.

**CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA ARDHI**

(1) Upungufu wa wafanyakazi wenye fani za kitaalamu

(2) Uchelewaji wa upatikanaji wa vibali vya ujenzi

(3) Ukosefu wa hatimiliki kwa nyumba zinazomilikiwa na wizara.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI**

(1) Kamati inashauri kuchukuliwa hatua za haraka katika kufanikisha suala la upatikanaji wa wafanyakazi wanaohitajika katika fani za kitaalamu kwenye wizara ili kuweza kusaidia kufanikisha majukumu ya wizara kwa ufanisi Zaidi.

(2) Kamati inasisitiza kufanyiwa kazi suala la upatikanaji wa vibali vya ujenzi ambalo limekua ni changamoto kwa sasa na kupelekea watu kujenga bila vibali kutokana na kusubiria muda mrefu lakini pia na Serikali kukosa mapato yatokanayo na vibali hivyo.

(3) Vile vile kamati inaendelea kuisisitiza wizara kufanya jitihada na kuhakikisha majengo yao yote yanapatiwa hatimiliki lakini pia na majengo yote yanayomilikiwa na Serikali pamoja na maeneo yapatiwe hatimiliki ili kuondosha changamoto ya uvamizi na migogoro iliyopo kutoka kwa wananchi.

**(a) PROGRAMU NDOGO YA URATIBU WA MIPANGO, SERA NA TAFITI ZA WIZARA**

Programu hii ndogo ina jukumu la kutekeleza shughuli za kuratibu/ kuandaa Mipango na Miongozo ya Kisera ya utekelezaji wa kazi za Wizara, kuratibu uandaaji na mapitio ya Sheria za Wizara pamoja na kuendeleza tafiti kwa ajili ya kuimarisha utoaji wa huduma katika Sekta za Wizara.

**(b) PROGRAMU NDOGO YA UTAWALA NA UENDESHAJI**

Programu hii inajukumu la kusimamia uendeshaji wa shughuli za kila siku za Wizara pamoja na uendelezaji wa Rasilimali Watu kwa kuandaa mipango ya kujenga uwezo wa Watumishi, kuratibu shughuli za Viongozi wa Wizara Kitaifa na Kimataifa, kutoa uelewa kwa wafanyakazi juu ya masuala ya mtambuka, kuimarisha mazingira bora ya kazi, kushughulikia haki na stahiki za Watumishi waliopo na waliomaliza muda wao wa utumishi kwa sababu mbalimbali, kuhakikisha kuwepo kwa watendaji wa kutosha na wenye sifa pamoja na kusimamia nidhamu kwa Watumishi wote wa Wizara na Taasisi zake.

**(c) PROGRAMU NDOGO YA URATIBU NA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA WIZARA PEMBA**

Programu hii ndogo inatekelezwa na Afisi Kuu Pemba na inajukumu la kuratibu na kusimamia utawala na mipango ya kazi za Wizara zinazotekelezwa Pemba ikiwemo Programu na Miradi ya Maendeleo.

**CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI WIZARA YA ARDHI PEMBA**

(1) Ufinyu wa bajeti ambao unapelekea kazi kutofanyika kwa ufanisi

(2) Upungufu wa wafanyakazi wataalamu kama vile wapimaji ardhi, wapangaji wa miji, Maafisa wa Ardhi, Wathamini wasaidizi wapimaji na mainjinia.

(3) Upungufu wa vitendea kazi kama vile magari, vifaa vya upimaji tatizo ambalo hupelekea ucheleweshaji wa kazi na kupungua ukusanyaji

mapato yatokanayo na upimaji na ramani, nyaraka za ardhi, muongozo wa matumizi ya Ardhi, kazi za uthamini na kodi za usajili wa ardhi.

(4) Uhaba wa maeneo mapya yakupangwa, kupimwa na kugawiwa kwa wananchi jambo ambalo linapelekea kupungua ukusanyaji mapato.

(5) Uchakavu wa baadhi ya nyumba za Serikali

(6) Kutolipa kodi kwa wapangaji katika nyumba za Serikali hususan wafanyakazi wa Taasisi za Serikali

**USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

(1) Kamati inashauri wizara kuongeza bajeti kwa Ofisi kuu Pemba ili iweze kutekeleza kazi zake kwa ufanisi pamoja na kununua vitendea kazi kama vile vifaa vya kupimia na magari.

(2) Kamati inashauri kutengwe fedha maalum kwa ajili ya matenngenezo ya nyumba Serikali katika bajeti ijayo.

(3) Ofisi iendelea kuchukua jitihada za makusudi kwa wapangaji wote wanaodaiwa kuweza kulipa kodi ili Serikali iweze kuingiza mapato lakini pia kuweza kutumika katika kufanya matengenezo ya nyumba hizo.

(4) Kamati pia inapendekeza kufanyiwa haraka suala la wafanyakazi wataalamu ili waweze kusaidia kuleta ufanisi katika kukamilisha majukumu ya wizara Pemba.

**3.3 PROGRAMU KUU YA USIMAMIZI WA ARDHI NA MAKAAZI**

Programu hii inajukumu la kuhakikisha usalama wa matumizi ya ardhi na huduma za makaazi bora kwa Wananchi na inajumuisha Programu ndogo mbili kama ifuatavyo: -

**(a) PROGRAMU NDOGO YA UTATUZI WA MIGOGORO YA ARDHI**

**MAHKAMA YA ARDHI**

Programu hii inatekelezwa na Mahakama ya Ardhi ambapo Mahakama ya Ardhi imeanzishwa kwa Sheria namba 7 ya mwaka 1994. Shughuli za msingi za Mahakama hii ni kupokea, kusikiliza na kuzitolea maamuzi kesi zinazotokona na migogoro ya ardhi zinazowasilishwa na wananchi pamoja na Taasisi mbalimbali.

**CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI MAHKAMA YA ARDHI**

(1) Bajeti ndogo ambayo haikidhi haja kwa shughuli za Mahkama ya Ardhi pamoja na kiwango kidogo cha upatikanaji wa fedha ambacho husababisha kutofikiwa malengo yaliyopangwa.

(2) Ufinyu wa jengo la Afisi Kuu Mwanakwerekwe

(3) Ukosefu wa vitendea kazi kama viti, meza, kompyuta nk

(4) Ukosefu wa usafiri kwa Unguja na Pemba

(5) Ukosefu wa posho nyeti la wafanyakazi wa Mahkama ya Ardhi

(6) Uwepo wa madeni makubwa ya wazee wa Mahkama kutokana na OC ndogo isiyotosheleza.

(7) Ukosefu wa Mashikiano kwa taasisi nyengine mfano Kamisheni ya Ardhi na Mipango Miji ambao wanapelekea kuwepo na migogoro ya ardhi isiyokua ya lazima.

(8) Kuwepo na changamoto katika sheria no 7 ya mwaka 1994 na kupelekea shida kwenye utekelezaji wake kwa baadhi ya maeneo.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI**

(1) Kamati inashauri kwa mwaka wa fedha ujao kutengwa fedha za kutosha kwa ajili ya uendeshaji wa Mahkama na kuingizwa kwa wakati ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

(2) Kamati inaendelea kushauri jengo linalomilikiwa na Zeco liliopo pembezoni mwa Mahkama ya Ardhi Mwanakwerekwe kupatiwa Mahkam ya Ardhi ili waweze kupunguza changamoto walonayo ya ufinyu wa ofisi hali ambayo inakwaza katika utendaji kazi.

(3) Kamati inasisitiza wizara kuchukua jitihada za makusudi kuhakikisha suala la ukosefu wa vitendea linatatulia ili kuweza kufanikisha majukumu ya Mahkama kwa uweledi.

(4) Kamati inashauri kuangaliwa kwa jicho la huruma Mahkama hii na kupatiwa usafiri ambao umekua ni changamoto kubwa kwao kwa Unguja na Pemba.

(5) Kamati inashauri Wizara kufatilia upatikanaji wa posho nyeti ambalo wanatakiwa kupatiwa wafanyakazi wa Mahkama ya ardhi kutokana na unyeti wa kazi zao ambazo zinalingana na kazi za Mahkama myengine.

(7) Kamati inaitaka Wizara kuhakikisha kuwepo na mashirikiano yakutosha kutoka katika taasisi zote ambazo kwa namna moja au nyengine zinahusika na masuala ya ardhi ili kuweza kuzuia na kupunguza migogoro ya ardhi ambayo kila siku imekua ni kilio katika nchi yetu na kusababisha athari mbalimbali kwa jamii.

(8) Kamati inaitaka Mahkama kufanya kazi kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizowekwa.

(9) Pia, kamati inashauri kesi za ardhi kusikilizwa na kupatiwa hukumu kwa muda mfupi ili kuepusha wahusika kupita njia zisizo sahihi kutokana na kesi kukaa muda mrefu hali ambayo inaleta zaidi changamoto na kuongezeka migongano isiyo ya lazima.

(10) Vile vile Mahkama ishirikiane na Kamisheni ya Ardhi na Serikali kwa kuwapatia wananchi ufumbuzi wa migogoro ya Ardhi.

(11) Kamati inashauri kufanyiwa marekebisho sheria ya Mahkama ya Ardhi namba 7 ya 1994 kama ilivyo rekebishwa na sheria namba 1 ya 2008 ili kuwezesha utatuzi wa migogoro ya ardhi kuwa kwa njia rahisi na kuondoa matumizi ya utaratibu mgumu unaotumika katika sheria ya mwenendo wa madai ambao husababisha kupoteza muda mwingi na badala yake kuanzisha utaratibu mwepesi unaojitosheleza katika kuendesha mashauri ya ardhi.

(12) Vile vile kamati inaitaka wizara kufatilia suala la kiwanja kiliopo nyuma ya Mahkama ya Koani ambacho wanataka kukitumia kwa ajili ya ujenzi kwa kuongeza maeneo ya Mhkama hiyo.

**(b) PROGRAMU NDOGO YA UTAWALA WA ARDHI NYUMBA NA MAKAAZI**

Programu hii ndogo ina jukumu la kuhakikisha usalama wa umiliki wa ardhi na uimarishaji wa huduma za makaazi kupitia upimaji wa ardhi, utambuzi na usajili wa ardhi, mipango ya miji na matumizi ya ardhi, ukarabati wa nyumba za maendeleo na majengo ya Serikali. Programu hii ndogo inatekelezwa na Taasisi zifuatazo: -

**(i) KAMISHENI YA ARDHI**

Kamisheni ya Ardhi imeanzishwa kwa Sheria Namba 6 ya Mwaka 2015. Lengo la kuanzishwa kwake ni kuleta ufanisi zaidi katika kusimamia Sheria za Sekta ya Ardhi pamoja na kuziunganisha Idara zote zinazosimamia matumizi na maendeleo ya ardhi.

**CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI KAMISHENI YA ARDHI**

(1) Uwepo wa kazi nyingi za upimaji wa maeneo ambayo yameshalipiwa kutokana na ukosefu wa fedha. Kamati imejuilishwa kuwa hali hii inasababishwa na mfumo wa malipo ambao unatumika kwa njia ya benki na malipo kuingia moja kwa moja katika mfuko wa Serikali na kupelekea kazi ya upimaji ifanyike kwa fedha za OC.

(2) Kuwepo kwa miongozo mbalimbali inayosimamia masuala ya ardhi kunapelekea kuongezeka kwa migogogoro ya ardhi.

(3) Upungufu wa vifaa vya upimaji ikiwemo GPS, usafiri na wataalamu.

(4) Kiwango kidogo cha uelewa wa jamii kuhusu masuala ya matumizi na dhana ya ardhi.

(5) Kuongezeka kwa uvamizi wa ardhi za Serikali, kilimo na eka 3.

(6) Kuwepo kwa ardhi kubwa ambayo bado haijafanyiwa utambuzi wa kusajiliwa kulingana na malengo ya usajili.

(7) Mazingira ya jengo la Kamisheni hayaridhishi na hayawezi kujenga morali ya kazi kwa watumishi wa Taasisi hii.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI**

(1) Kamati inashauri Kamisheni ya ardhi kufanya mashirikiano na Taasisi mbalimbali katika kutunza na kuendeleza masuala ya ardhi ikiwemo Mahkama ya Ardhi, ZAWA, Mamlaka ya Serikali za Mitaa pamoja na wahusika wa Mipango Miji na Vijiji.

(2) Kamati inashauri Kamisheni kutoa elimu kwa umma juu ya masuala yote ya Ardhi ili kuepusha migogoro isiyo ya lazima katika jamii.

(3) Kamati pia inashauri kamisheni kupitia Wizara kufanya marekebisho ya sheria zao ambazo zinakwaza katika utekelezaji wa majukumu yao.

(4) Aidha, kamati inashauri Wizara kuliangalia suala zima la changamoto kubwa ya usafiri kwa afisi zake za Unguja na Pemba.

(5) Kamati inasisitiza kuchukuliwa hatua za haraka suala la uvamizi wa ardhi za Serikali, kilimo na eka 3 ili kuepusha athari za kimazingira pamoja na upotevu wa ardhi kiholela usiozingatia sheria na taratibu zilizowekwa.

(6) Pia, kamati inapendekeza kupitia Wizara kuangalia utaratibu mzuri wa upimaji maeneo ambayo yameshalipiwa kwa kuangalia njia ambayo wataweza kuzipata fedha zilizokwisha kulipwa ambazo zinatakiwa kutumika katika kazi ya kupima maeneo hayo.

(7) Vile vile kamati inashauri kuangaliwa suala la jengo la Kamisheni na kuchukuliwa hatua zinazofaa.

(8) Kamati inatoa wito kwa Wizara kupitia Kamisheni kuhakikisha wananchi wote waliolipa kupimiwa wanapimiwa ili kuondosha malalamiko yaliopo kwa wananchi kutokana na kuchukua muda mrefu bila kupata huduma hii.

**(ii) OFISI YA MTHAMINI MKUU WA SERIKALI**

Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali imeanzishwa kwa Sheria Namba 5 ya mwaka 2015 kwa dhumuni la kuhakikisha usimamizi mzuri wa kazi za

uthamini kwa Serikali, Sekta binafsi na wananchi kwa ujumla. Kazi kuu ya Mthamini Mkuu ni kuthibitisha kazi za uthamini zinazofanywa nchini na wathamini wa Taasisi za Serikali na Kampuni binafsi.

**CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI OFISI YA MTHAMINI MKUU WA SERIKALI**

(1) Uhaba wa bajeti

(2) Kuwepo na mapungufu katika mfumo wa uingizaji taarifa za ripoti za uthamini ikiwepo kukosekana kwa baadhi ya vifaa. (server na upatikanaji wa internate)

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI**

(1) Kamati inashauri Serikali kupitia wizara kuwapatia bajeti itakayowasaidia kutekeleza kazi walizojipangia na kupatiwa kwa wakati.

(2) Kamati inaishauri Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali kupitia wataalamu kutumia taaluma zao vizuri na kuishauri Serikali.

(3) Kamati pia inasisitiza kukamilishwa mfumo wa kieletroniki uliotaarishwa kwa lengo la kuingiza taarifa za mali zilizofanyiwa uthamini ili kuwe na rikodi rasmi ambayo itasaidia kuhifadhi taarifa zote za kazi zinazofanywa na Ofisi ya Mthamini Mkuu lakini pia kusaidia kuwepo kwa taarifa ambazo kwa sasa zinakosekana.

**(iii)WAKALA WA MAJENGO ZANZIBAR**

Wakala wa Majengo imeanzishwa kwa Tangazo la Kisheria (Legal Notice) namba 50 ya mwaka 2017. Lengo la kuanzishwa Wakala wa Majengo ni kutoa huduma ya Makaazi kwa Viongozi Wakuu, Maafisa Wakuu Waandamizi wa Serikali na Watumishi wa Umma. Aidha, Wakala wa Majengo ina wajibu wa kusimamia na kuratibu miradi ya ujenzi na matengenezo ya majengo ya Serikali ili kuhakikisha ubora wa majengo hayo.

**CHANGAMOTO ZINAZOKABILI WAKALA WA MAJENGO**

(1) Ukosefu wa fedha za kutekelezea majukumu waliojipangia
(2) Ukosefu wa Ofisi. Hadi sasa Wakala wa Majengo haina Ofisi yake wenyewe bali inatumia jengo la ZSSF waliloazimwa liliopo Kilimani.
(3) Wakala kukabidhiwa nyumba za Serikali ambazo ni chakavu zinazohitaji matengenezo makubwa
(4) Upungufu wa vitendea kazi pamoja na teknolojia za kisasa
(5) Miradi mingi ya Serikali bado haipitii kwa Wakala wa Serikali
(6) Kuwepo na uelewa mdogo kwa baadhi ya Taasisi za Serikali juu ya majukumu ya Wakala wa Majengo katika usiamamizi wa nyumba za Serikali.
(7) Ukosefu wa wafanyakazi kama Mwanasheria, Mshika fedha na mtu wa ufatiliaji na tathmini.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI**

(1) Kamati inashauri Serikali kupitia Wizara kuwapatia fedha katika bajeti ili waweze kutekeleza majukumu yao.
(2) Pia, kamati inaisisitiza wizara kuchukua jitihada za makusudi ma kulifanyia kazi suala la kuwapatia ofisi Wakala wa Majengo.
(3) Vile vile, kutokana na umuhimu wa Taasisi hii kamati inaona ni vyema wakapatiwa vitendea kazi ambavyo vitawawezesha kufanikisha majukumu yao ipasavyo.
(4) Kamati inatoa wito kwa Serikali kuwatumia Wakala wa Majengo katika miradi yao ili waweze kutoa ushauri kiutaalamu na kuweza kusaidia kufanikiwa kwa miradi hiyo na kuwa na ubora.
(5) Kamati pia, inashauri kutolewa elimu kwa Taasisi zote za Serikali juu ya umuhimu wa kuwepo Taasisi hii na majukumu yake ili ziweze kusaidia kufanikisha lengo lililokusudiwa.
(6) Kamati inaitaka wizara kuchukua hatua za kupatikana wafanyakazi wenye upungufu katika Taasisi hii ambao ni muhimu kuweza kufanikisha utendaji kazi wa ofisi.

**(iv)SHIRIKA LA NYUMBA ZANZIBAR**

Shirika la Nyumba Zanzibar (ZHC) limeanzishwa kwa Sheria namba 6 ya mwaka 2014. Lengo la kuanzishwa Taasisi hii ni kuwawezesha Wananchi kupata makaazi bora na salama pamoja na kuziimarisha nyumba za Shirika zilizopo na kujenga nyumba mpya. Kamati imebahatika kutembelea Shirika la Nyumba pamoja na kukagua nyumba mbali mbali zinazomilikiwa na Shirika. Pia imeweza kutembea Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) na kujifunza mambo mbali mbali.

**CHANGAMOTO ZINAZOKABILI SHIRIKA LA NYUMBA**

(1) Kuwepo kwa madeni makubwa kwa wapangaji wa shirika jambo ambalo linasababisha kukosekana fedha na kucheleweshwa kwa utekelezaji wa mipango ya Shirika ya ujenzi wa nyumba mpya na matengenezo ya nyumba zilizopo.

(2) Utunzaji mbovu wa nyumba za Serikali kwa wapangaji wanaoishi katika nyumba za Shirika.

(3) Ukosefu wa hatimiliki kwa nyumba za Shirika.

(4) Uhaba wa fedha za kufanyia matengenezo nyumba ambazo baadhi yake ni mbovu sana na zinahitaji fedha nyingi kufanyiwa marekebisho.

(5) Ukosefu wa wataalamu wa fani za ujenzi ikiwemo wahandisi ujenzi, wabunifu majengo na wakadiriaji majengo.

(6) Kuwepo kwa nyumba nyingi chakavu ambazo zimerithiwa kutoka kwa iliyokua idara ya nyumba na Maendeleo ya Makaazi.

(7) Ukosefu wa usafiri kwa ajili ya kufatilia shughuli za Ofisi

(8) Matumizi mabaya ya nyumba za Shirika ikiwemo kupikia kuni, kufuga kuku na bata, kufanya marekebisho kwa kuvunja baadhi ya sehemu ya nyumba ambayo hayaruhusiki kufanywa na kupelekea kuondosha uimara wa nyumba hizo na kukodisha kwa watu wengine tofauti na anayejulikana na Shirika na kwa bei ya juu.

(9) Mazingira machafu katika maeneo ya nyumba za shirika.

(10) Uwepo wa nyumba ambazo zimeshamaliza muda wake kimatumizi ambazo pia ni chakavu na hatarishi.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI**

(1) Kamati inaendelea kuwashauri Shirika kuchukua hatua na mbinu mbadala katika kuhakikisha wale wote wanaodaiwa kulipa ili Shirika liweze kuinuka na kutekeleza kazi zake ikiwemo ukarabati wa nyumba. Lakini pia kamati inalitaka shirika kuchukua jitihada mbadala kuhakikisha deni kutoongezeka.

(2) Kamati haikufurahishwa na suala la ukosefu wa hatimili za nyumba za Shirika hivyo, inaitaka wizara kuchukua jitihada za ziada kuweza kuzipatia nyumba zote za Shirika hatimili.

(3) Kamati inashauri pia kuchukuliwa hatua za upatikanaji wa wataalamu za fani za ujenzi ambao watasaidia sana kuweza kushauri na kufanikisha majukumu ya Shirika.

(4) Kamati imesikitishwa na uwepo wa matumizi mabaya ya nyumba yanayofanywa na wapangaji hao ambayo yameharibu na kuleta hasara kwa Shirika, hivyo kamati inalita Shirika kuandaa muongozo maalum utakaoonesha utaratibu mzima wa ukaaji katika nyumba hizo na kwa atakaeshindwa kuweza kuchukuliwa hatua ikiwemo kuondoshwa katika nyumba izo, lengo kuweza kuondosha tabia ya uharifu unaofanywa na wakaazi wa nyumba hizo ambao umeashaathiri nyumba na kuipa hasara Serikali.

(5) Kamati inashauri katika bajeti ijayo kuangaliwa suala la usafiri ambalo ni muhimu sana katika ufatiliaji wa majukumu ya Shirika ya kila siku.

(6) Vile vile kamati inalitaka Shirika kwa kushirikiana na Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Halmashauri na Masheha kuhakikisha suala la usafi katika mazingira ya nyumba za Shirika linapewa kipaumbele.

(7) Kamati pia inaitaka wizara kuliangalia na kulichukulia hatua zinazofaa suala la nyumba zisizofaa kimatumizi ili kuepusha athari kwa wakaaji na Serikali kwa ujumla.

(8) Kamati inaendelea kusisitiza Uhakiki wa wapangaji uwe endelevu ili kuweza kuwatambua wapangaji wote pamoja na kuhakikisha wateja wao wote kuwa na mikataba.

**ZIARA YA KAMATI KWA SHIRIKA LA NYUMBA LA TAIFA (NHC)**

Kamati pia katika kufanya kazi zake ilipata fursa ya kutembelea Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) na kujifunza mambo mbali mbali ambayo yameliwezesha Shirika kupiga hatua kimaendeleo.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI**

1. Kamati imebaini kwamba Shirika la Nyumba Tanzania linaendelea kupiga hatua kubwa ya kimaendeleo katika sekta ya ujenzi na nyumba, hivyo kamati inaishauru Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kuweka mikakati imara katika kupanga mipango bora ya matumizi ya ardhi ili kuendeleza sekta ya ujenzi na makaazi bila ya kuathiri ongezeko la idadi ya watu.
    - Kuweka masharti ya ujenzi wa kwenda juu (ghorofa) badala ya kuendelea na majengo ya kutambaa.
    - Kuunganisha viwanja na kujenga majengo makubwa ya ghorofa
    - kutanua wigo na ubunifu wa Shirika la Nyumba la Zanzibar.
2. Kutafuta hatimiliki ya majengo ya Shirika la Nyumba ili kupata dhamana ya mikopo na kufanya miradi mengine ya kimaendeleo.
3. Wataalamu wa Shirika la Nyumba wafanye utafiti wa kina kuhusiana na mahitaji ya makaazi kwa sasa na baadae.

Vile vile Kamati katika kutekeleza majukumu yake imeweza pia kukutana na Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba, Bodi ya Kondominio na Bodi ya Usajili Wasanifu Wahandisi na Wakadiriaji Majengo na kuweza kupata yafuatayo: -

**(a) BODI YA KUDHIBITI KODI ZA NYUMBA**

Bodi ya kudhibiti Kodi za Nyumba imeanzishwa kwa Sheria ya Kudhibiti Kodi za Nyumba Sura ya 98 ya mwaka 1953 (CAP 98 of 1953). Lengo la

kuanzishwa kwa Bodi hii ni kusikiliza na kuzitolea maamuzi kesi zinazotokana na migogoro ya upangishaji wa nyumba za Serikali na nyumba binafsi.

**CHANGAMOTO ZA BODI YA KUDHIBITI KODI ZA NYUMBA**

(1) Ukosefu wa ofisi, kamati imeelezwa hadi sasa Bodi hii haina ofisi yakufanyia kazi na inatumia chumba cha kuazima kilichopo katika Ofisi ya Bodi ya Uhaulishaji Ardhi Zanzibar.
(2) Uhaba wa fedha kwa malipo ya vikao vyake ambapo kila mwezi inalazimika kufanya vikao Unguja na Pemba.
(3) Mrundikano wa madeni ya muda mrefu kwa malipo ya vikao.
(4) Ukosefu wa usafiri
(5) Ukosefu wa mtaalamu wa utatuzi wa migogoro

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI**

(1) Kamati inaishauri wizara kuangalia uwezekano wa kupatiwa ofisi na usafiri kwa Unguja na Pemba ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi.
(2) Kamati inashauri kutolewa elimu kwa jamii kuhusiana na masuala ya kodi za nyumba ili wapate uelewa.
(3) Pia kamati inaishauri wizara kufanya jitihada za kupatikana mtaalamu wa utatuzi wa migogoro ili aweze kusaidia kufanikisha lengo la bodi hii.
(4) Kamati inaishauri Wizara kuhakikisha inachukua hatua za makusudi katika kuondokana na madeni ambayo yamekua ni changamoto ya muda mrefu yanayoathiri utendaji kazi wa bodi hii.

**(b) BODI YA KONDOMINIO**

Bodi hii imeanzishwa kwa Sheria ya Kondominio namba 10 ya mwaka 2010. Lengo la kuanzishwa Bodi ya Kondominio ni kusajili, kuratibu na kusimamia matumizi ya pamoja kwa majengo yenye sehemu zinazomilikiwa na watu tofauti.

**CHANGAMOTO ZA BODI**

(1) Ukosefu wa usafiri

(2) Upungufu wa wataalamu ikiwemo wataalamu wa kada za uhandisi, ukadiriaji majengo, uthamini, mkaguzi wa hesabu na afisa manunuzi.

(3) Ufinyu wa eneo la ofisi za bodi

(4) Kukosekana kwa usimamizi mzuri wa nyumba za maendeleo

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI**

(1) Kamati inaitaka wizara kuiangalia bodi kwa mwaka wa fedha ujao kuwaptia usafiri na wataalamu wakutosha ili kuweza kutekeleza majuku yao kwa ufanisi na kufikiwa malengo yaliyokusudiwa ya kuwepo bodi hii.

(2) Pia, kamati inaishauri wizara kushughulikia suala la kulifanyia matengenezo jengo linalotumiwa na bodi ili waweze kuwa na sehemu zakutosha kufanyia kazi kwa kuwatengea bajeti maalum ya kukarabati jengo.

(3) Vile vile kamati inaishauri bodi wajifunze zaidi kwa wenzao nje ya Zanzibar ili iweze kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

**(c) BODI YA USAJILI WASANIFU WAHANDISI NA WAKADIRIAJI MAJENGO**

Bodi hii imeanzishwa kwa Sheria ya Usajili wa Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo namba 5 ya Mwaka 2008. Lengo la kuanzishwa kwa Bodi hii ni kusimamia, kudhibiti na kuwaendeleza wataalamu wa ujenzi ili wafanye kazi zao kwa utaalamu na viwango vinavyotakiwa.

**CHANGAMOTO ZA BODI**

1. Kutojisajili kwa baadhi ya wataalamu wa kigeni hasa wale wanaofanya kazi katika miradi ya maendeleo inayofadhiliwa na washirika wa maendeleo.
2. Wataalamu waliosajiliwa kuchelewa kulipa ada yam waka
3. Mapungufu ya sheria iliyopo ambayo haikutaja baadhi ya fani ushirikishwaji wa wahandisi katika fani ya barabara, umeme, mitambo na nyenginezo

4. Bodi kushindwa kuwaendeleza wahitimu waliosajiliwa na bodi kutokana na ukosefu wa fedha.
5. Ukosefu wa jengo la ofisi za bodi

## WIZARA YA MAJI NISHATI NA MADINI

## 4.0 MUUNDO WA WIZARA

Wizara ya Maji, Nishati na Madini inaundwa na Idara nne na Taasisi tatu. Idara na taasisi hizo ni: -

1) Idara ya Mipango, Sera na Utafiti,
2) Idara ya Nishati na Madini,
3) Idara ya Utumishi na Uendashaji
4) Ofisi ya Afisa Mdhamini Pemba.
5) Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA),
6) Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO)
7) Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati (ZURA).

### 4.1 MALENGO YA WIZARA

Lengo kuu la Wizara ni kutoa huduma nafuu, endelevu na zilizo bora kwa wananchi wote katika mazingira yanayofaa kuleta ufanisi katika utoaji wa huduma za maji, nishati na madini.

### 4.2 PROGRAMU ZA WIZARA

Kamati ilifuatilia kwa karibu sana utekelezaji wa Programu Kuu za Wizara ya Maji, Nishati na Madini ambazo ni; -

1) Programu ya Usimamizi wa Huduma za Maji
2) Programu ya Usimamizi wa Huduma za Nishati na Madini
3) Prograamu ya Uendeshaji na Uratibu wa Mipango ya Wizara

### 4.3 PROGRAMU YA USIMAMIZI WA HUDUMA ZA MAJI

Kamati ilipata fursa ya kupokea taarifa za Utekelezaji pamoja na kutembelea baadhi ya maeneo ya utekelezaji wa program hii ambayo inatekelezwa na Idara ya Maji pamoja na Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA).

**(a) MAMLAKA YA MAJI ZANZIBAR (ZAWA)**

Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) imeanzishwa chini ya Sheria Namba 4 ya Mwaka 2006 kama ilivyopendekezwa katika Sera ya Maji ya Taifa ya Zanzibar ya Mwaka 2004, ikiwa na jukumu la kuhakikisha upatikanaji wa maji safi na salama pamoja na kulinda na kuhifadhi rasilimali maji.

**CHANGAMOTO ZA MAMLAKA YA MAJI (ZAWA)**

Pamoja na taarifa mbali mbali za utekelezaji wa ZAWA na Idara ya Maji, Kamati ilitaka kujiridhisha na taarifa hizo na hatimae ikaamua kufanya ziara katika vijiji mbali mbali vya Unguja na Pemba kwa kila Wilaya ambapo kwa ujumla Kamati imebaini changamoto kadhaa za ZAWA pamoja na Sekta ya maji kwa ujumla kama ifuatavyo: -

**(a) Tatizo la Uzalishaji na Uvunaji maji.**

i. Kamati imebaini kwamba ZAWA inakabiliwa na tatizo kubwa la Uzalishaji wa Maji Safi na salama ambapo kwa sasa imefanikiwa kuzalisha asilimia 55% tu kulingana na shabaha zake suala ambalo linachangiwa na uchache wa visima vya kuzalisha maji kulingana na mahitaji na ongezeko la idadi ya watu hivi sasa.

ii. Mbali na uhaba wa visima bado ZAWA inakabiliwa na tatizo la Miundombinu ya vyanzo vya Maji ambavyo takriban vyote viko chini ya ardhi.

**(b) Tatizo la Miundombinu ya kutosha na Uhifadhi wa Maji**

i. Vilevile Kamati imebaini kwamba ZAWA inakabiliwa na tatizo la uhaba wa Mabomba.

ii. Aidha Kamati imegundua kuwa pia kuna tatizo kubwa la uhifadhi wa nishati ya maji katika matangi machache yaliyo ambayo pia yameshaanza kuchakaa.

**(c) Mtandao wa Maji**

i. Kufuatia ziara ya Kamati katika vijiji mbali mbali, Kamati imebaini kwamba bado kuna sehemu na vijiji kadhaa havijafikiwa na huduma ya maji safi na salama.

**(d) Mvunjo na Kuchakaa kwa Mabomba.**

i. Kamati imeshuhudia Maji mengi yakipotea njiani kutokana na Mivujo inayochangiwa na kuchakaa kwa mabomba yaliyopo ambapo kwa

mujibu wa wataalamu wa ZAWA kunabaadhi ya mabomba yamewekwa tangu 1923. Aidha suala jengine linalochangia mivujo hiyo ni pamoja na uungaji mbovu na wakiholela wa huduma ya maji hasa vijijini

**(e) Madeni:**

i. Kamati imebaini kuwa kuna madeni makubwa kutoka kwa Taasisi za Serikali. Aidha kuna mwamko mdogo wa wananchi kulipia huduma ya maji.

**(f) Ufinyu wa Bajeti :**

i. Ufinyu wa Bajeti ya fedha za miradi ya maendeleo inapelekea maeneo mbali mbali kukosa miradi ya maji na Mamlaka kushindwa kununua mashine za kusukumia maji kwa mujibu wa mpango wao, hivyo kushindwa kutoa huduma za maji safi na salama katika maeneo mbali mbali ya mijini na vijijini.

**(g) Uvamizi wa maeneo ya Vianzio vya Maji**

i. Kamati imeripotiwa juu ya kuendelea kwa changamoto ya uvamizi wa maeneo ya Vianzio vya maji, licha ya kwamba mengi ya maeneo hayo yanalindwa muda wote

**ZIARA YA KAMATI MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA DAR ES SALAAM (DAWASA)**

Kamati ilitembelea DAWASA na kushuhudia mafanikio makubwa ya Mamlaka hiyo. Miongoni mwa mafanikio Hayo ni kama yafuatayo:_

a) DAWASA imefanikiwa kutoa huduma kwa wakaazi wa Dar es Salaam kwa asilimia 92.
b) Kuwaingiza wateja wao wote katika mfumo wa Kidigitali suala ambalo linawapa wepesi wa kufahamu taarifa zao kwa wakati
c) Kuingia katika mfumo wa kimtandao ili kujua taarifa zote za vianzio vya maji na miundombinu ya maji.
d) DAWASA imekuwa ikizibadilisha mita kongwe ili kupata *reading* za uhakika .

**MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI.**

1. Kamati inaishauri Wizara kupitia Mamlaka ya Maji Zanzibar kuwa na mpango wa kutumia Maji ya ZAWA kwa matumizi ya kawaida tu na ya kijamii, na sio shughuli nyengine za biashara na uzalishaji kama vile Matofali, kilimo, ukoshaji wa vyombo vya moto, na mengineyo.

2. Wizara iwe na utaratibu wa kufanya utafiti wa kutosha kabla ya kuanza miradi mikubwa ya maji ili kujiepusha na usumbufu na hasara zinazoweza kujitokeza wakati wa utekelezaji wa miradi hiyo.

3. Kamati inaiagiza ZAWA kuingia katika mifumo ya kisasa ili hatimae iweze kugundua hitilafi katika vianzio na miundombinu yake ya maji badala ya kusubiri kupewa taarifa na wananchi.

4. Kamati inashauri kuwa, visima vikongwe vya maji ambavyo vilitelekezwa na ZAWA vifufuliwe ili kusaidia upatikanaji wa maji vijijini.

5. Kamati inaishauri na kuiagiza Wizara kubadilisha mfumo wa mabomba uliopo hivi sasa na kuweka mabomba madhubuti, imara na yenyekukidhi mahitaji ya muda mrefu ili kupunguza tatizo la mivujo linaloendelea kutokea kila sehemu na kupunguza gharama za ununuzi wa mabomba kila baada ya kipindi kifupi.

6. Vile vile kamati inashauri Wizara kufanya utafiti ili kubaini sababu zinazopelekea pampu za maji kuungua mara kwa mara na kusababisha kukosekana kwa huduma hiyo kwa baadhi ya maeneo.

## 4.4 PROGRAM KUU YA USIMAMIZI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MADINI

### (a) SHIRIKA LA UMEME ZANZIBAR (ZECO)

Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) lililoanzishwa kwa Sheria Nambari 3 ya Mwaka 2006 ni miongoni mwa taasisi muhimu katika kuunga mkono jitihada za Serikali ya kuwapatia huduma ya umeme wananchi wake na hivyo kuinua hali za wananchi na kuongeza uchumi wa Taifa. Shirika hili linajukumu la kuzalisha, kusambaza na kuuza umeme kwa wananchi wa Zanzibar.

**CHANGAMOTO ZA SHIRIKA LA UMEME ZANZIBAR (ZECO)**

1. Ufinyu wa Bajeti

2. Uharibifu wa miundombinu ya umeme ikiwemo wizi wa nyaya

3. Uwepo wa madeni makubwa kwa Taasisi za SMZ na SMT

4. Kuwepo na umeme mdogo kwa maeneo mengi ambapo ni changamoto kwa watumiaji.

Vile vile kamati ilitembelea na kukaguwa Vituo vikuu vya Kusafirisha na kupokea nishati ya umeme kutoka Gridi ya Taifa Tanzania Bara kuja Zanzibar kupitia njia ya bahari.

**a) Kituo cha Mkumbuu Wesha.**

Kamati pia ilijulishwa kwamba kituo cha kupokea umeme kutoka Tanga hadi Pemba kwa njia ya bahari cha Mkumbuu na kushuhudia hali halisi ya kituo hicho.

**Changamoto.**

- ✓ Tatizo la miundombinu ya barabara hasa wakati wa mvua suala ambalo wakati mwengine linapelekea walinzi kupelekwa kwa njia ya bahari.

**c) Kituo cha Ras Kiromoni.**

Kamati ilitembelea kituo cha umeme cha Ras Kiromoni kinachopokea umeme kutoka Gridi ya Taifa kupitia Kituo cha Tageta Dar es Salaam na hatimae kusafirishwa kuja Zanzibar kupitia kituo cha Fumba kwa kutumia line mbili ziliopo kituoni hapo.

Kamati imebaini kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa ikigharamia upatikanaji na uendeshajiwa miundombinu ya kusafirisha umeme takriban kilomita 37.5 kutoka Ubungo kupitia Kituo cha Tageta, Ras Kiromoni hadi Zanzibar tokea mwaka 1979 hadi hivi sasa.

**Utafiti wa Kamati.**

Katika ziara hii Kamati imebaini yafuatatyo:-

1. Line namba 1 ni kongwe na ya muda mrefu takriban miaka 40 sasa kulingana na ongezeko kubwa la mahitaji ya nishati ya umeme pamoja na uwezo (capacity) wa line hiyo.

2. Katika line namba 2 (Line Mpya) Kamati imegundua kwamba pia line hiyo imekuwa ikitumika kwa mawasiliano ya Kampuni ya Simu ya Zantel pamoja na Mkongo wa Taifa kupitia Fiber ya ZECO ndani ya Line hiyo.

**Kikao cha Kamati na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO)**

Kamati ilikutana na watendaji wakuu wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) ambalo miongoni mwa majukumu yake ni kuuza umeme kwa jumla (bulk supply) kwa Shirika la Umeme la Zanzibar.

Kwa mujibu wa takwimu za TANESCO umeme uliouzwa kwa ZECO kwa kipindi cha Julai-Disemba 2021 umeongezeka kwa asilimia 7.8% ikilinganishwa na wateja wengine wa upande wa Bara. Hali hii inaonesha kuwa mahitaji ya umeme Zanzibar yanaongezeka kwa kasi hivyo kuna haja ya kuangalia kama miundombinu inayoleta umeme inaweza kukidhi ongezeko hilo.

**Hali ya sasa ya Deni la Umeme la ZECO**

Kamati iliarifiwa kwamba hadi kufikia Disemba 2021 deni halali ambalo ZECO wanalikubali kulipa TANESCO ni shilingi **7,084,506,602.65.**

Aidha Kamati imebaini kuwa katika kikao cha Menejiment za TANESCO na ZECO tarehe 23/12/2021 kilichofanyika Dar es Salaam ilijulishwa kuwa Bodi ya Wakurugenzi ya TANESCO iliidhinisha bei ya kuuza umeme kuwa **shilingi 130.0 kwa Unit Moja** kama ilivyokubaliana katika pande zote mbili lakini bodi ya wakurugenzi ya ZECO bado haijakaa kujadili na kuidhinisha bei iliyopendekezwa.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI**

1. Kamati inashauri Shirika kuzidi kujipanga katika kuboresha nishati ya umeme ambayo mahitaji yanaongezeka siku hadi siku.

2. Kamati inalitaka Shirika la Umeme kubadilika na kwenda na wakati kwa kuboresha miundombinu yake ikiwemo ununuzi wa transfoma zitakazotoa huduma bora kwa watumiaji wengi na kuachana na tabia ya kuwekwa transfoma ndogo baada ya muda mfupi hazitoshelezi na kuweka nguzo imara na kuwa na utaratibu wa kuzikagua mara kwa mara kabla kuleta athari.

3. Kamati inashauri shirika la umeme kutumia nguzo za zege badala ya nguzo za miti kwa bajeti ijayo ili kuepeusha changamoto ziliopo sasa

za kuoza kwa nguzo nyingi na kuleta athari ambapo inatokana na nguzo hizo kuvunwa zikiwa changa.

4. Vile vile kamati inaisisitiza Wizara kupitia Shirika kuhakikisha wanafatilia wadaiwa wote wa Taasisi za Serikali ili kusawazisha madeni yao na kuliwezesha shirika kutoa huduma bora Zaidi.

5. Pia, kamati inalitaka Shirika kuimarisha kitengo chake cha huduma kwa wateja ikiwa ni njia moja wapo yakuboresha huduma zitolewazo na Shirika.

6. Kamati inaishauri Wizara kuhakikisha kuwa Bodi ya Wakurugenzi ya ZECO inakaa kuridhia bei ya **shilingi 130.0 kwa Unit Moja** ili baadae iwasilishwe EWURA kwa ajili ya kuidhinishwa na kuanza kutumika.

7. Wizara kupitia Shirika la Umeme la Zanzibar kuendelea kutoa elimu kwa wananchi wanaofanya shughuli zao za kijamii na wanaozunguka ndani ya maeneo ya miundombinu ya umeme.

8. ZECO iendelee kutoa ulinzi katika miundombinu yake yote ili kujiepusha na uharibifu unaoweza kujitokeza.

**MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA MAJI NA NISHATI (ZURA)**

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) imeanzishwa chini ya Sheria Namba 7 ya mwaka 2013. Aidha, Nishati zinazosimamiwa na Mamlaka ni Umeme, Mafuta, Gesi Asilia na Nishati nyengine yoyote inayozalisha umeme. Pia, katika sekta ya Maji, Mamlaka inasimamia udhibiti wa maji safi na maji machafu.

**CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI MAMLAKA**

i. Muundo wa Mamlaka ambao hauakisi utekelezaji wa majukumu ya Mdhibiti ni changamoto kubwa katika utendaji wa kazi za kila siku wa Mamlaka.

ii. Mgongano wa majukumu baina ya Wizara ya Maji, Nishati na Madini na Mamlaka (ZURA).

iii. Kuongezeka na kutolipwa kwa wakati gharama za uendeshaji wa majengo ya Mamlaka kwa taasisi zilizokuwemo ndani ya majengo zikiwemo umeme, maji, ulinzi, usafi, matengenezo ya

muda maalum (Genereta, Lifti, Viyoyozi na Miundombinu ya maji).

iv. Mamlaka zinazodhibitiwa na ZURA (ZECO na ZAWA) kutopeleka mrejesho kwenye maombi ya leseni pamoja na changamoto mbali mbali zinazowasilishwa kufuatia na kaguzi mbali mbali za ZURA katika taasisi hizo.

**Ukaguzi wa ZURA katika Mamlaka ya maji Zanzibar.**

Kamati imeripotiwa kwamba ZURA imefanya ukaguzi wa miundombinu ya Maji kwa kukaguwa visima 59 ili kujua ufanisi wake. Kufuatia ukaguzi huo changamoto mbali mbali zimeibiliwa ikiwemo: -

i. Kukosekana kwa uzio, vifaa vya usalama katika vituo vya maji (pump house), pamoja na mazingira machafu sana kwa baadhi ya vituo na baadhi ya visima kutokua na mifuniko sehemu ya juu (Well Head).

ii. Uwepo wa makaazi ya watu karibu na vyanzo vya maji.

iii. Kutofanya kazi kwa baadhi ya visima kutokana na kuungua kwa pump.

iv. Ufungaji ovyo wa Wanyama katika maeneo ya vyanzo vya maji.

v. Uchakavu wa miundombinu ya maji kwa baadhi ya visima.

Kwa upande mwengine Kamati imepokea taarifa ya Mamlaka ianyohusu ukaguzi wa vituo vitano (5) vya kupozea umeme kwa ajili ya kulisha katika maeneo ya Mazizini, Jangombe, Bambi, Kilimahewa, Dole na Maruhubi pamoja na maeneo yote ya mjini. Kufuatia ukaguzi huo ZURA imebainika kuwa: -

i. Kituo cha Mwanyanya kipo karibu na jaa mita tano tu kutoka kituoni.

ii. Vituo vyote havina kisanduku cha huduma ya kwanza.

iii. Kituo cha Mpendae kinahitaji kuwekewa vipoza joto kama vile feni, Aircondition au feni za kutolea hewa nzito nje.

iv. Vituo vya Mpendae na Welezo tayari vimezidiwa ambapo hupelekea mpaka transfoma zake kuzima kipindi cha matumizi makubwa ya umeme.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI**

i. Kamati inaiagiza na kuishauri Wizara kufuatilia hatua ya Mamlaka ya kuwasilisha Muundo mpya unaoakisi majukumu ya Mdhibiti huko Kamisheni ya Utumishi wa Umma.

ii. Pia Kamati inashauri ZURA na Wizara kwa ujumla zikae pamoja na kutafuta mshauri elekezi wa kuweza kupambanua baina ya majukumu ya Wizara na Mamlaka ili kuondoa mkanganyiko uliopo sasa ambao unapelekea kuvizisha utendaji katika majukumu.

iii. Kamati haikuridhishwa na tabia ya ZECO na ZAWA kutopeleka mrejesho kwa ZURA kwa kaguzi wanazofanya, hivyo basi Kamati inazitaka Taasisi hizo kufanya mrejesho wa ripoti zinatolewa na ZURA.

iv. Kamati inaishauri Wizara kukaa na Taasisi zote zinazotumia majengo ya ZURA na kukubaliana jinsi ya kuchangia katika gharama za uendeshaji wa majengo hayo.

**IDARA YA NISHATI NA MADINI.**

Idara ya Nishati na Madini imeanzishwa kwa uwezo wa Rais wa kuanzisha taasisi ikiwa na jukumu la kusimamia rasilimali za nishati na madini na huduma zake.

**Ziara ya Kamati katika Bohari ya kuhifadhia mafuta.**

**Bandari ya Wesha:**

Kamati ilitembela Bohari Kuu ya kuhifadhia mafuta ya Pemba huko Wesha na kushtushwa na hali iliyoikuta ya Bohari hiyo iliyojengwa miaka mingi iliyopita ambapo kwa sasa inapokea wastani wa meli 2-3 kwa mwezi kutoka Tanga.

**Changamoto**

**a) Miundombini Chakavu**

- ✓ Kamati imebaini kwamba Matangi ya kuhifadhi mafuta yaliyopo katika Bohari hiyo yameshachakaa na yameanza kuzibwa zibwa huku ikiwa tayari yamemaliza muda wake wa matumizi. Vilevile Kamati imepokea taarifa za kitaalamu zinazoonesha kwamba matangi hayo yanaweza kufumka wakati wowote ambapo uwezo wake

kwa sasa umeanza kupungua kwani yanahifadhi lita 300,000 badala ya lita 600,000.

**b) Tatizo la Usalama wa kiafya, kimazingira na kiulinzi.**

- ✓ Kutokana na miundombinu chakavu ya sehemu hiyo wafanyakazi na wageni wanaotembelea eneo hilo wanakabiliwa na tatizo la usalama wa afya zao na pia wanafanyakazi kwa wasiwasi muda wote.
- ✓ Shughuli za kibinadamu zinazoendelea pembezoni mwa Kituo zinapelekea changamoto ya kimazingira
- ✓ Uzio uliozingushwa katika baadhi ya maeneo ya kituo hautoshelezi katika suala zima la kiulinzi.

**c) Masafa baina ya Tank moja na jengine**

- ✓ Wataamalu wa sehemu hiyo waliieleza Kamati kwamba Matangi ya kuhifadhia mafuta yamekaribiana sana suala ambalo linatia wasiwasi pale inapotokea dharura ya kuyakarabati na wanahisi ni rahisi mno kukolezana pale inapotokea hitilafu.

**d) Matumizi na Shughuli za Kibinadamu**

- ✓ Kamati imeshuhudia kuwepo kwa njia na shughuli za kibinadamu kama vile kilimo, ufugaji na uvuvi katika maeneo yanayozunguka Bohari hiyo suala ambalo Kamati inadhani sio sahihi kulingana na unyeti wa sehemu hiyo.

**e) Kupungua kwa kina cha maji**

- ✓ Kamati vile vile imeshuhudia kupungua kwa kiasi kikubwa kina cha maji katika Bandari ya Wesha hali ambayo inaweza kupelekea mtihani kwa meli kubwa kufunga nanga katika gati hiyo.

**f) Uwezo mdogo wa matangi ya kuhifadhia mafuta**

- ✓ Kamati imejulishwa kwamba kutokana na Ongezeko kubwa sana la matumizi na mahitaji ya Nishati ya Mafuta huko Pemba kwa sasa matangi hayo ya kuhifadhia mafuta ni kidogo na hayatoshelezi.

**Bohari ya Mtoni**

Kamati pia ilitembelea Bohari ya Mtoni ambayo nayo inakabiliwa na tatizo la uwepo wa shughuli za kijamii kama ilivyo katika Bohari ya Wesha.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

1) Kamati inaishauri Serikali iangalie uwezekano wa kujenga Matangi mapya kwa lengo la kukabiliana na changamoto iliyopo ya uchakavu wa Miundombinu ya kuhifadhi nishati ya mafuta kulingana na ongezeko la mahitaji ya nishati hiyo.

2) Kamati inazishauri taasisi zote zinazohusika na Bohari za Wesha na Mtoni kushirikana kwa pamoja na hatimae kulipatia ufumbuzi suala shughuli za kibinadamu katika maeneo yanayozinguka maeneo hayo.

# SEHEMU YA TATU

## HITIMISHO

### 5.0 HITIMISHO

Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati ya Baraza la Wawakilishi inawapongeza kwa dhati Mawaziri, Makatibu Wakuu, pamoja Viongozi na watendaji wote kwa Ujumla wa Wizara zote tatu zinazosimamiwa na Kamati hii kwa mashirikiano makubwa waliyoipatia Kamati kwa kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu yake ya Kikatiba na Kikanuni.

Aidha, Kamati inatoa shukurani za kipekee kwa Maafisa Wadhamini wa Wizara hizi pamoja na wasaidizi wao wote kwa mashirikiano mazuri waliyoipatia Kamati wakati wote Kamati ilipokuwa Kisiwani Pemba katika kutekeleza majukumu yake.

Vilevile, Kamati inatambua, kuthamini na Kushukuru ushirikiano ulipata kutoka kwa Ofisi ya Uratibu wa Shughuli za SMZ suala mbalo lilipelekea kufanikisha shughuli zake zilizojipangia huko Tanzania Bara kwa ufanisi mkubwa.

Mwisho, na kwa umuhimu mkubwa Kamati inampongeza kwa dhati Spika wa Baraza la Wawakilishi Mhe. Zubeir Ali Maulid, Naibu Spika Mhe. Mgeni Hassan Juma, Katibu wa Baraza la Wawakilishi Ndg. Raya Issa Msellem, Afisa Mdhamini Afisi ya Baraza la Wawakilishi Pemba ndugu Abdulghani Abdullah Said na Mratibu wa Kamati Ndg. Khamis Hamad Haji pamoja na sekretariati yote ya Baraza la Wawakilishi kwa kuiwezesha vyema Kamati kutekeleza majukumu yake na kuweza kutayarisha Ripoti yake kwa mwaka 2021/2022. Kamati inashauri mashirikiano hayo yaendelezwe kwa kipindi chote kinachofuata.